24. THE RED BADGE OF COURAGE

24. THE RED BADGE OF COURAGE

Karibu kwenye muhtasari wa riwaya inayoitwa THE RED BADGE OF COURAGE iliyoandikwa na STEPHEN CRANE ikihusu vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Marekani ambapo mwanajeshi mpya anakimbia mapigano kwa sababu ya hofu, ila baadaye anarudi kwenye mapigano na kuwa shujaa.

👉1
Wanajeshi wako kwenye kambi eneo ambalo lina baridi kali.
Wamekuwa hapo kwa kipindi kirefu bila ya kuwa na mapambano.
Kumekua na tetesi mbalimbali kwamba mapambano yataanza lakini hilo halitokei.
Siku moja mwanajeshi anayeitwa Jim anawaambia wenzake amepata taarifa za uhakika kwamba kesho yake kutakuwa na mapambano.
Wengi hawamwamini maana tetesi hizo zimekuwa nyingi.
Jim anawaambia taarifa zake ni kutoka chanzo cha uhakika na kama hawaamini wasubiri mpaka siku ya kesho, watajionea wenyewe.

Mmoja kati ya wanajeshi hao ni kijana anayeitwa Henry, kwa kusikia taarifa hizo anatoka na kwenda kwenye hema lake.
Anakumbuka siku aliyojiunga na jeshi, alimwambia mama yake kwamba anataka kujiunga ila akamkatalia, akamwambia ni bora kwake kubali shambani kwao kuliko kwenda vitani.
Lakini hadithi za vita zilimhamasisha sana na akaenda kujiandikisha bila ya ruhusa ya mama yake.
Aliporudi na kumweleza mama yake kwamba ameshajiandikisha hakusema maneno mengi, bali alimwambia mapenzi ya Mungu yatimizwe.
Akiwa anamuaga mama yake anamuasa sana awe makini, asiende kutaka ushujaa na kufanya mambo ya hatari kwake. Asikie anayoambiwa na afuate maelekezo.
Pia anamtahadharisha aangalie sana marafiki anaokuwa nao, anamwambia jeshini kuna wengi wenye tabia zisizo nzuri, akijihusisha nao na yeye ataharibikiwa.

Safari ya mafunzo na mazoezi kuelekea uwanja wa vita inamfanya Henry ajione ni shujaa na anakwenda kufanya makubwa.
Maneno ya hamasa na sifa wanayopewa, jinsi wengine wanavyowachukulia inamfanya ajione ana mengi ya kufanya kwenye taifa lake.
Lakini sasa amepata taarifa kwamba mapambano yanakwenda kuanza kesho na hofu kubwa imemuingia.
Hana uhakika kama ataweza kuhimili mapambano hayo au atakimbia. Anagundua katika kipindi chote alikuwa anajipa tu moyo, ila sasa unafika wakati wa mapambano na kutambua hakuwa na maandalizi sahihi katika kujiamini.

Henry anamuuliza Jim iwapo mapambano yatakuwa makali, anamjibu huenda yakawa makali sana.
Anamuuliza tena anawachukuliaje wanajeshi wapya, je watayaweza mapambano? Anajibu japo wanajeshi wengine wanawadharau, anaona wanaweza kupambana vizuri tu.
Henry anamuuliza tena iwapo anafikiri kuna wanajeshi wapya ambao watakimbia. Jim anamjibu kwenye kila kundi huwa hawakosekani watu wa aina hiyo.
Henry anamuuliza kama yeye Jim aliwahi kufikiria kukimbia alipokuwa mwanajeshi mpya. Jim anamjibu alipokuwa mwanajeshi mpya alijipa msimamo huu, kama wote watakimbia basi na yeye atakimbia. Ila hata kama mmoja atabaki akipambana na yeye atabaki akipambana.
Maneno hayo yanamfanya Henry ajisikie angalau na hofu aliyokuwa nayo inapungua.

👉2
Siku iliyofuata wanagundua taarifa ya Jim haikuwa sahihi, mapambano hayakuanza kama alivyosema.
Wengi walimlalamikia kwa kuwadanganya.
Lakini bado Henry aliendelea kuteseka ndani yake na hali ya kutokujiamini kama anayaweza mapambano.
Alijaribu kuongea na wanajeshi wengine ili kuona kama wana wasiwasi kama wake, kitu ambacho hakukiona. Lakini alijipa moyo kwamba wanajaribu tu kuficha hayo.
Kila alipomuuliza Jim alionekana kumwamini kwamba atapambana vizuri tu, kitu ambacho pia hakukiamini sana.
Wakati mwingine alijikuta akikasirikia uongozi mzima wa jeshi kwa kuwaweka kwa muda mrefu eneo moja bila ya mapambano.
Wakati wanajeshi wengine wakionekana kuzoea hilo, yeye lilimchosha sana.

Siku moja anakuja kiongozi wa ngazi za juu wa jeshi na kuongea na kiongozi wa kikosi chao. Watu wanapata matumaini kwamba mapambano yanaanza.
Wanatoka asubuhi na mapema kabla ya jua kuchomoza na kutembea kwa umbali mrefu kuelekea uwanja wa mapambano.
Wanatembea siku nzima mpaka giza linapoingia na wanapiga kambi.
Henry anatumia muda mwingi akiwa peke yake, bado akiteseka na hali ya kutokuwa na uhakika kama atayaweza mapambano.
Anakumbuka alipokuwa nyumbani, jinsi alivyozifanya kazi za shamba na kuhudumia mifugo.
Anatamani sana angeweza kurudi kwenye maisha yale, anajiona hakuwa sahihi kuingia kwenye jeshi, maana siyo sehemu sahihi kwake.
Akiwa peke yake, mwanajeshi mwenzake mpya aitwaye Wilson anakuja na kumuuliza ana tatizo gani mpaka anakaa peke yake, Henry anajibu anafikiria tu.
Henry anamuuliza Wilson iwapo atapambana bila kukimbia, Wilson anamjibu ndiyo, atapambana bila ya kukimbia.
Henry anamwambia lakini wapo wengi wanaosema hivyo ila muda wa mapambano unapofika wanakimbia. Wilson anajibu ni kweli, ila yeye ameshajiambia atapambana na hatokimbia.
Henry anamwuliza anadhani yeye ni mtu jasiri kuliko wote? Wilson anamjibu kwa hasira hajasema yeye ni jasiri kuliko wote, ila atapambana. Anaondoka na kumwacha.
Henry anazidi kujisikia vibaya, maana haoni kama kuna mwingine anapitia hali kama yake. Anaona wote wamejitoa kupambana bila kukimbia, ila yeye tu ndiye mwenye wasiwasi.

👉3
Siku inayofuata wanaamka na kuendelea na safari, wanasikia milio ya risasi kwa mbali na hapo Henry anaona kifo chake kimekaribia.
Hofu kubwa inamjia, anagundua kwamba hakuchagua kujiunga na jeshi kwa matakwa yake, bali kwa ushawishi mkubwa uliotengenezwa na serikali.
Wanaendelea kuzunguka lakini hakuna mapigano.
Henry anakasirishwa zaidi na hilo, anaona kama uongozi wa kikosi hauna mpango wowote. Anaona lengo ni kuzungushwa tu na hakuna mapambano. Anaona hilo ni hatari pia, kwani adui anaweza kuwavamia na kuwaua.
Anapata hamasa kubwa ndani yake ya kwenda kumkabili kanali na kumweleza hayo, pia anataka awaambia wanajeshi wengine hatari iliyo mbele yao.
Lakini kadiri wanavyozunguka na kuchoka, anaona hawezi kutimiza hilo.
Anamlalamikia Jim kwamba kwa nini wanazungushwa hivyo, Jim anamjibu ni moja ya mbinu za kivita, kutokukaa eneo moja kwa muda mrefu.
Henry anamwambia haoni ni sawa kuwazungusha wanajeshi na kuwachosha badala ya kuwapeleka uwanja wa mapambano.
Jim anamwambia bado ni mgeni kwenye jeshi, kuna mengi hajui.

Henry anazidi kupatwa hasira, anaona kama hali itaendelea hivyo bora atoroke kwenye hicho kikosi na kwenda kukabiliana na maadui mwenyewe.
Anaona bora ajipeleke kwenye kifo kuliko kuendelea kuzunguka hivyo.
Lakini kadiri wanavyoendelea kuzunguka, huku akizoea eneo hilo na kuchoka, ndivyo anavyoona hakuna umuhimu wa utekeleza anachofikiri.
Mwanajeshi mmoja anamfuata Henry na kumpa pochi yake akimwambia anapata hisia pambano hilo litakuwa la mwisho kwake, anamtaka awape ndugu zake pochi hiyo.

👉4
Wanafika eneo ambalo palikuwa na mapambano makali.
Wanakuta baadhi ya wanajeshi wa vikosi vingine wakiwa wameumia, huku wengine wakiwa wamekimbia.
Hali hiyo inamfanya Henry aone hata yeye anaweza kukimbia pia akijikuta kwenye hali kama hiyo.

👉5
Wanajeshi wapya wanapewa maelekezo ya mapambano na kupaswa kufuata maagizo wanayopewa.
Mapambano ni makali, baadhi ya wanajeshi wa kikosi cha Henry wanapigwa risasi na kufa.
Henry bado anaendelea na mapambano japo hofu bado imemjaa.

👉6
Wanapambana mpaka wanafanikiwa kumshinda adui, hakuna tena majibizano.
Henry anajisikia vizuri, anaona ameweza kupambana mpaka mwisho bila kukimbia.
Wanajiambia ni muda wa kupumzika sasa maana hakutakuwa na mapambano mengine siku za karibuni.
Kabla hawajatulia wanasikia sauti ikisema vikosi vya adui vinakuja tena.
Wengi hawaamini wanachosikia, wanajua kwa hali waliyonayo hawawezi kupambana na kikosi kingine kipya bila msaada.
Baadhi ya wanajeshi wanaanza kukimbia, Henry anataka kubali lakini anaona kama atabaki mwenyewe.
Anajiunga nao na wanakimbia, wanakwenda mwendo mrefu.
Henry anakaribia kitu ambao jenerali yupo, anatamani aende kumwambia ni jinsi gani watu wako kwenye hatari kama wataendelea kupambana.
Lakini kabla hajaenda anasikia jenerali akituma mtu aende kumwambia kapteni waendelee na mapambano.

👉7
Henry anaendelea kukimbia na anagundua kwamba wanajeshi wachache waliobaki wamepambana na kushinda.
Yeye alikimbia kwa kuwa alijua kwa uchache wao wasingeweza kushinda.
Kitendo cha wachache hao kuweza kushinda kinamuumiza, anajiona huenda hakuwa sahihi.
Ila anajipa moyo kwamba wameshinda kwa bahati tu. Kwa vyovyote vile maamuzi ya busara yalikuwa kusitisha kwanza mapigano, kwenda kujipanga na kurudi kwenye mapambano wakiwa na nguvu zaidi.
Anajiambia baadaye hilo litakukuja kujulikana.
Anaendelea kukimbia katikati ya pori na kuona jinsi asili inaendesha mambo yake kwa amani na utulivu mkubwa, anajiambia hivyo ndivyo maisha yanapaswa kuwa.
Anafikiria atawakabilije wanajeshi wenzake atakaporudi kambini. Anaona hayupo tayari kwa hilo na kuendelea kukimbia.

👉8
Henry anaendelea kukimbia na sasa anasikia sauti za mapambano mengine makubwa kuliko aliyoyaacha.
Anaona ni bora aelekee yalipo mapambano hayo.

Anafikiria jinsi walivyokuwa wanaona mapambano yao ni makubwa kumbe hayakuwa kitu ukilinganisha na mapambano mengine yanayoendelea.
Anafika eneo la mapambano, waliokufa ni wengi na wengine wengi wameumia.
Wale walioumia wanaugulia maumivu huku wakilaumu na kutukana uongozi dhaifu wa jenerali ambao ndiyo umepelekea maafa yote hayo.
Henry anawakaribia baadhi ya wanajeshi wenye majeraha ambao wanaeleza jinsi mapambano yalikuwa makali na wakajitoa kupambana bila ya kukimbia.
Mwanajeshi mmoja anamuuliza Henry yeye ameumizwa wapi, anaondoka ili asimuone.

👉9
Kadiri Henry anavyopita katikati ya wanajeshi wengine anagundua kila mmoja ana majeraha ya risasi isipokuwa yeye tu.
Anawaonea wivu na kutamani naye angekuwa na jeraha la risasi, maana ni ishara ya ujasiri.
Henry anaendelea kutembea katikati ya wanajeshi hao na anakuta mwanajeshi ambaye anakataa asisaidiwe, anamkaribia na kugundua ni Jim, ana majeraha makubwa ya risasi.
Henry anamwambia atamsaidia, Jim anamwambia amuache maana hali yake ni mbaya.
Henry anamwambia hawezi kumuacha, anamsaidia kumuinua na kumsaidia atembee.
Jim anamwambia kitu pekee anachohofia ni kuanguka barabarani halafu akanyagwe na vifaru.
Jim anapata nguvu ya ajabu na kuacha barabara, anakimbilia kwenye pori. Henry anamfuata ila Jim anamwambia amuache mwenyewe kwa muda.
Henry anamuacha, Jim anasogea mbele zaidi na kusimama kwa utulivu mkubwa, kisha anatoa sauti kali ya maumivu na kuanguka chini.
Henry anamsogelea na kumkuta anakakamaa, anakata roho.
Henry anaondoka akiwa na uchungu zaidi baada ya kumpoteza mwanajeshi pekee aliyekuwa karibu naye.

👉10
Mmoja wa wanajeshi aliyekuwa na Henry wakati Jim anakufa anaendelea kufuatana na Henry.
Yeye ana majeraha kichwani na amekuwa anaongea sana, akimuuliza Henry maswali mbalimbali.
Henry anagundua mwanajeshi huyo pia ameanza kupoteza kumbukumbu na ni ishara atakufa muda siyo mrefu.
Henry anaamua kuachana naye na kuondoka.
Ndani yake anajiona ana hatia, akishuhudia wengine waliopambana wanakufa huku yeye aliyekimbia akiendelea kubaki hai.

👉11
Henry anafikiria kurudi kwenye kikosi chake na kuendelea kupambana.
Anaona hatua aliyochukua ya kukimbia ni ha aibu na hiyo itamuandana maisha yake yote.
Lakini anajipa moyo kwamba alioona hatari mapema na hivyo kuchukua hatua sahihi.
Anafikiria maelezo atakayokwenda kutoa ili wenzake wamuamini, lakini kwa kila anachofikiria anaona udhaifu ulio ndani yake.
Anaona hata wakimsikiliza hawatamuamini na hata wakimuamini, wakati mwingine wa mapambano watakuwa na wasiwasi naye wakijua atakimbia muda wowote.
Pamoja na hayo anachagua kurudi kwenye kikosi chake.

👉12
Henry anatekeleza azimio lake la kurudi kwenye kikosi chake, japo hajui atakipataje.
Anaendelea kwenda na anaungana na wanajeshi wengine, ambao hawaonekani kujali au kumsaidia.
Anaumia mguu wakati anakimbia, anatafuta wa kumsaidia hapati.
Anaendelea kwenda na maumivu, huku akifikiria kama akae mahali kwanza au aendelee kwenda.
Akiwa anaenda anakutana na mwanajeshi ambaye anakuwa tayari kumsaidia, anamuuliza kikosi chake anamtajia.

Mwanajeshi huyo anamwambia hadhani kama kikosi hicho kilikuwa kwenye mapambano siku hiyo.
Anamwambia jinsi siku ilivyokuwa ngumu kwa kila kikosi.
Anamsaidia mpaka anafika mahali na kumuonesha moto unaowaka, anamwambia pale ndipo kikosi chako kilipo. Anamuaga na kumwacha aende peke yake.

👉13
Henry anafika kwenye kambi ya kikosi chake na kumkuta Wilson akiwa kwenye lindo.
Wilson anashangaa kumuona, anamwambia alifikiri ameshakufa.
Henry anamwambia amepitia magumu mengi, amepigwa risasi ya kichwa pia na amepambana sana mpaka kuweza kufika hapo.
Wilson anampeleka kwenye hema lake, wanajeshi wengine pia wanakuja na kumpa pole Henry kwa yaliyomkuta.
Wilson anampa huduma ya kwanza, anamkagua kichwa na kumkuta ana jeraha dogo.
Anamfunga kwa kitambaa na kumwambia alale mpaka kukuche ndiyo apate huduma zaidi.
Wilson anamsifu Henry kwa kuendelea licha ya kupigwa risasi, kwani wengine wasingeweza kuendelea, wangekuwa hospitali.
Wilson anamuacha Henry alale kwenye kitanda chake.

👉14
Henry anaamka akiwa amepunguz uchovu aliokuwa nao, anaona kama amelala miaka elfu moja.
Wilson anamuuliza anajisikiaje asubuhi hiyo, anaangalia kidonda chake na kukigusa, Henry analalamika kwa maumivu.
Wanajeshi wengine wanaamka pia, wanazungumzia mapambano waliyopitia, Henry anawaambia Jim amekufa, wengi hawaamini.
Mkuu wa kikosi hicho anamweleza Henry kwamba walidhani nusu ya wanajeshi wao wameuawa, lakini wamekuwa wanarudi mmoja mmoja kama yeye, hivyo wengi hawajafa kama walivyodhani.

👉15
Wakiwa wanasubiria pambano jingine linalokaribia kuanza, Henry hajisikii tena hofu kama kipindi cha nyuma.
Yale aliyopitia yamempa uzoefu mkubwa na amegundua mtu huwezi kujiandaa vya kutosha kwenye mapambano ya kivita. Bahati ina nafasi kubwa na hivyo mtu unapaswa kuikabili hali kadiri inavyokuja.
Pia anaona hakuna anayejua siri yake kwamba alikimbia, hivyo machoni pa wengine anaonekaba shujaa na ataendelea kujichukulia kuwa shujaa hivyo.
Anaona pia huu ni wakati mzuri wa kuondoka jeshini na kurudi nyumbani.
Atapokelewa kama shujaa na simulizi zake zitasikilizwa na kuaminiwa na wengi japo hazitakuwa sahihi.
Anoana hilo pia litamfurahisha mama yake na kumpa ufahari.

👉16
Kikosi cha Henry wanaenda kwenye mapambano mengine.
Henry anaendelea kulaumu uongozi mbovu wa jenerali ambao unapelelea jeshi kuzidi kupoteza huku wao wakizungushwa zungushwa bila ya sababu.
Henry anajisahau na kujikuta anajisifia kwamba kikosi chao cha wanajeshi wapya kimeonesha ushujaa na kupambana bila ya kukimbia.
Mwanajeshi mmoja anamuuliza kama anadhani yeye ni mpiganaji hodari sana, kauli hiyo inamshtua sana Henry na anakaa kimya.
Luteni wa kikosi chao anawaambia waache kupoteza muda kubishana mambo yasiyo na tija, kazi yao ni kupigana na wafanye hiyo.

👉17
Kikosi kinaendelea na mapambano, bado Henry ana hasira kubwa juu ya viongozi wa jeshi na namna

wanavyoshindwa kuyapanga mapambano vizuri.
Anaona wao wanachukuliwa kama wanyama wanaopelekwa machinjoni.
Hilo linampa hasira ya kupambana zaidi na anapiga risasi nyingi na kwa muda mrefu kuliko wanajeshi wengine.
Wanajeshi wote wanamshangaa kwa namna anavyopambana kwa hasira. Luteni anamwambia angekuwa na wanajeshi elfu moja kama yeye, vita ingeisha ndani ya wiki.
Luteni anasifia na kusema hatakuja kupata kikosi cha wanejeshi wapya kama wao.
Henry anachukuliwa kama shujaa kwa namna anavyopambana kwa hasira bila kujali au kuchoka.
Hilo linampa sifa na anajikuta akiwa mbele zaidi ya wengine katika mapambano.

👉18
Mapambano ni makali na joto ni kali, wanajeshi wanapatwa na kiu kali.
Henry na mwenzake Wilson wanatoka kwenda kutafuta maji ya kunywa.
Wanazunguka lakini hakuna chanzo cha maji.
Wakiwa wanarudi kwenye kikosi chao wanapita karibu na alipo jenerali, wanamsikia akitoa maagizo kwa mwanajeshi kwamba kuna vikosi vya adui ambavyo viko karibu na ni hatari.
Anamuuliza kikosi gani kwa upande wao bado kina nguvu, anamjibu kikosi namba 340 ambacho ndipo alipo Henry.
Jenerali anamwambia akakiandae kikosi hicho kwa mapambano hayo makali na anamwambia hadhani kama wengi watapona.
Henry na mwenzake wanaangaliana kwa mshangao kwa kile walichosikia.
Walirudi kwenye kikosi wanawaeleza wengine ambao hawaamini, lakini mwanajeshi aliyetumwa anafika na kuwapa taarifa.
Wanalipokea hilo, japo Henry na mwenzake ndiyo wanaojua hatari kubwa iliyo mbele yao, kwamba wengi hawatapona.

👉19
Kikosi kinaondoka kwenda eneo jipya la mapambano.
Henry anatangulia mbele huku akiwa anakimbia, wenzake wanamuona ni kama amechanganyikiwa.
Anapanda kwenye mlima na kuanza kupiga risasi hivyo, kitu kinachowashtua maadui na wanaanza kujibu mashambulizi.
Kanali anamtaka atoke hapo na waondoke maana siyo sehemu sahihi ya kuendeshea mapambano yao.
Henry anakuwa mgumu, hataki kuondoka ila analazimishwa na wanaondoka.

👉20
Mapambano yanakuwa makali, baadhi ya wanajeshi wanakimbia huku wengine wakijeruhiwa na risasi.
Kanali ni mmoja wa waliojeruhiwa na risasi mkononi, ila hajali hilo, anaendelea na mapambano.
Henry bado ana hasira kali, kila akikumbuma mazungumzo ya jenerali wakati anatuma maelekezo akijua kabisa wengi wanaenda kufa.
Kadiri wanavyopambana, ndivyo nguvu ya adui inavyokuwa kubwa zaidi.
Sehemu kubwa ya wanajeshi wanakata tamaa na kuona hawana tena cha kufanya, kwani adui amewazidi nguvu.

👉21
Licha ya kuzidiwa nguvu, kikosi cha Henry kimapambana sana, wanapigana kwa ujasiri licha ya kuwa wachache.
Wanafanikiwa kuwashinda maadui na wanakimbia.
Wanapumzika wakisimuliana jinsi mapambano yalivyokwenda.
Henry na Wilson wamekaa mbali wakizungumza.
Anakuja mjumbe wa jenerali na kuleta taarifa kwa kanali. Anamwambia jenerali hajafurahishwa na

matokeo yao, alitegemea wasonge mbele zaidi.
Kanali anamwambia hajali aliyesema hivyo ni nani, kama hawezi kuthamini kazi kubwa iliyofanyika basi ni mpumbavu.
Anasema wamepambana sana kuweza kushinda vikosi vya adui, hilo linapaswa kuthaminiwa.
Mjumbe huyo anamuuliza kanali kijana aliyekuwa amebeba bendera ni nani, anamjibu ni Henry.
Mjumbe anamwambia jenerali amesema kijana huyo pamoja na mwenzake wanatakiwa kupandishwa cheo kwa kazi kubwa waliyoifanya.
Henry na Wilson wanapelekewa taarifa hizo, wanafurahi sana na kusahau yote waliyokuwa wanalalamikia.

👉22
Henry sasa anayaangalia mapambano kama kiongozi.
Yuko eneo ambalo anaona pande zote zinazopambana.
Anaona jinsi vikosi vya upande wake vilivyozidiwa nguvu.
Lakini anajiambia hayupo tayari kusitisha mapambano.
Bado ana hasira ya kutaka kuonesha namna sahihi ya kuendesha mapambano.
Lakini vikosi vya upende wake vimezidiwa sana, wengi wanapigwa risasi na kufa.

👉23
Wengi wanataka mapambano yasitishwe kwa kuwa wamezidiwa nguvu.
Lakini Henry anaona ni hatari kusitisha mapambano kwa eneo ambalo wapo, itakuwa hatari zaidi kwani vikosi vya adui vimewazunguka.
Anaenda mstari wa mbele kwenye mapambano akiwa amebeba bendera, anaongoza mapambano na wanajeshi wanapata hamasa kubwa.
Wanapigana kwa ujasiri mkubwa na kuweza kuvishinda vikosi vya adui.
Wanafanikiwa kukamata mateka wengi kutoka vikosi vya adui.
Baada ya pambano kukamilika kwa mafanikio makubwa, Henry na Wilson wanakutana na kupongezana kwa kazi kubwa iliyofanyika.

👉24
Wanajeshi wote wanashangilia ushindi mkubwa ambao wameupata.
Lakini Henry haonekani kuwa na furaha, anakumbuka wakati alipotoroka jeshi na kushuhudia wengine wakifa mbele yake, hasa Jim na hilo linamuumiza sana.
Analia kwa uchungu, Wilson anamuuliza tatizo ni nini, hujibu ila anaendelea kulia.
Baadaye anaamua kuyaacha hayo yaliyopita, anatafakari yote aliyofanya mpaka sasa na kuona amekuwa na mchango mkubwa.
Anachagua kuyaacha makosa aliyofanya kwani hata akiyakumbuka sasa hayana msaada wowote.
Kwa kuchagua kuachana na hayo, anapata furaha kubwa.

👉25
Henry akiwa mzee anaongea na watu ambao wamekuja kusikiliza simulizi za vita kwake.
Kila mtu anajua ushujaa wake wakati wa vita na cheo cha juu alichopata kwa uhodari wake.
Henry yuko na mjukuu wake anayeitwa Jim, ambaye anapenda kuwa na babu yake kwa ushujaa wake.
Mmoja wa watu waliokuwa wanamsikiliza anamuuliza kama amewahi kuhofia wakati wa vita.
Henry anajibu ndiyo, wanacheka kwa kuwa hakuna aliyetegemea jibu hilo.
Henry anawaeleza pambano lake la kwanza alipatwa na hofu kubwa, aliposikia milio ya risasi alidhani yote inamlenga yeye.
Aliona kama ni mwisho wa dunia na hakuweza kuhimili, hivyo akakimbia.
Anawaambia baadaye alizoea hali hiyo na kupata ujasiri wa kuendelea na mapambano.
Wengi wanafurahishwa na uwazi wake wa kueleza ukweli.
Wakati wanaondoka mjukuu wake anamuuliza kama aliyosema ni kweli, Henry anamjibu ni kweli tupu.

Mjukuu huyo anaonekana kujisikia vibaya, alitegemea babu yake awe shujaa ambaye hajawahi kuhofia.

Wanarudi nyumbani, akiwa amelala usiku Henry anasikia kelele, kuamka anakuta mabanda ya ng'ombe na farasi yanawaka moto.
Anaingia na kuweza kuwaokoa wanyama wote, anatoka nguo zake zikowa zimeshika moto.
Wanamwagia maji kuzima moto huo, anaonekana kuwa na ujasiri wa hali ya juu.
Wanakumbuka kuna ndama ambao hawajatolewa, ila sasa moto umeshakolea sana.
Henry anataka kwenda kuwaokoa ndama hao ila watu wanamzuia, anajitoa kwa nguvu na kuingia kwenye banda lenye moto.
Kuingia tu paa la banda hilo linaanguka na moto mkubwa unafunika kabisa banda hilo.
Kila mtu anajua moto huo umemmeza kabisa Henry.

👉TUNAYOJIFUNZA.
Riwaya hii ambayo inaelezea mkasa wa kivita, ina mengi sana ambayo tunaweza kujifunza na kuyatumia kwenye maisha yetu.
1. Tumeona umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kusikiliza sauti ya ndani yako badala ya wale wanaokuzunguka. Henry alizuiwa na mama yake asijiandikishe kwenye jeshi, lakini kwa kuwa nk kitu kilikuwa kinatoka ndani yake, alichagua kufanya hivyo.
2. Tumejifunza pia hata unapofanya maamuzi kwa kusikiliza sauti yako ya ndani, bado baadaye utayajutia maamuzi hayo, hasa pale mambo yanapokuwa magumu. Tunaona Henry akijutia kujiunga na jeshi pale anapoingia kwenye mapambano ya kwanza na kujawa na hofu kubwa.
3. Unapokuwa mgeni kwenye kitu chochote, hofu huwa inakutawala uanpokaribia kukifanya. Henry alitawaliwa na hofu kubwa kipindi chote cha mwanzo na alijaribu kudadisi wengine ila hakuona wakiwa na hofu kama yeye.
4. Hofu inaweza kukusukuma kufanya maamuzi yasiyo sahihi, lakini unaweza kuyabadili na ukafanya kilicho sahihi. Usibaki kwenye makosa uliyofanya kwa sababu ya hofu uliyokuwa nayo kabla hujawa na uzoefu. Henry alikimbia lakini baadaye akachagua kurudi kwenye mapambano.
5. Ni rahisi kumlaumu kiongozi kwa maamuzi yake unapokuwa mfuasi. Lakini ukiwa kiongozi, kuna vitu unaona ambavyo wafuasi hawawezi kuviona na hivyo kupelekea ufanye maamuzi ambayo hayawezi kueleweka na wote. Henry alikuwa akimlaumu sana jenerali akiona hawezi kuliongoza jeshi, lakini alipopandishwa cheo ndiyo alijionea mwenyewe jinsi ufanyaji wa maamuzi unvyohitaji uwe tayari kuikabili hatari.
6. Hatupaswi kuficha makosa yetu ya nyuma ili kulinda sifa zetu, kwa kufanya hivyo tunaishia kuwapotosha wengine na wanaweza kutumia taarifa zisizo sahihi kufanya mambo na wakakosea. Henry aliamua kuweka wazi makosa yake, licha ya ushujaa wake, mwanzo alikuwa na hofu na ilimpelekea mpaka akakimbia.
7. Tumejifunza pia umuhimu wa marafikia ambao mnaelewana vizuri, Wilson alikuwa sehemu muhimu kwenye ujasiri wa Henry.
8. Kuwa na taarifa za ndani kunakusaidia kuipima vizuri hatari iliyo mbele yako. Henry aliweza kupambana kwa ushujaa baada ha kumsikia jenerali akisema jinsi hatari ilivyo kubwa kwa kikosi chao.
9. Njia pekee ya kuikabili hofu ni kufanya kile unachohofia. Kilichompa ushujaa Henry ni kuikimbilia hofu yake, kile alichohofia basi alikifuata mara moja. Alihofia mapambano na hivyo yalipotangazwa alikuwa wa kwanza kuyakimbilia. Kwa namna hiyo alipata nguvu ya kuweza kupambana na kuleta matokeo mazuri.
10. Ujasiri ni muhimu, lakini mtu unapaswa kupima hatari ya kitu kabla ya kukifanya na siyo tu kukifanya kwa sababu wewe ni jasiri. Henry anakufa kwenye moto kwa sababu ya ujasiri wake, kitu ambacho kisingetokea kama angepima vizuri hatari iliyo mbele yake.

Uchambuzi huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani, kupata chambuzi za vitabu vingine vizuri tembelea;
www.t.me/somavitabutanzania

Kupata vitabu vizuri vya Kiswahili vya maendeleo binafsi na mafanikio, weka app ya SOMA VITABU TANZANIA, fungua; www.bit.ly/somavitabuapp